**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA.**

**SHULE YA SEKONDARI MCHUCHUMA,**
**S.L.P.43,**
**LUDEWA.**
**13 MAY 2026.**

**MKUU WA SHULE 0756524162/0776524162 MAKAMU MKUU 0657179419/0717719949 MHASIBU 0714245966**

**Ndugu ………………………………………………**
**Mzazi/ Mlezi wa ……………………………………  S.L.P**
**………………………………………………..**

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI MCHUCHUMA WILAYA YA LUDEWA MKOA WA NJOMBE MWAKA ••••••••••••••••••••**

**1.0 Utangulizi**

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha TANO katika shule hii mwaka 2026/2027. Tahasusi (combination) ya ……. Shule ya sekondari Mchuchuma ipo katika Mkoa wa Njombe wilaya ya Ludewa kata ya Luilo, kijiji cha Kipangala umbali wa km 44 kutoka makao makuu ya halmashauri ya wilaya ya Ludewa. Usafiri wa basi kutoka kituo cha mabasi Njombe unapatikana saa 12:00 asubuhi, saa nne asubuhi kwa usafiri wa basi la Ibu Trans, (Nauli ya kutoka Njombe hadi Mchuchuma shule ilipo ni Tsh. 24000/=). Au Nauli ya kutoka Njombe hadi Ludewa Tsh. 19000/= na kutoka Ludewa hadi Mchuchuma Shule ilipo ni Tsh 7,000/= Kutoka Songwe na Mbeya unaweza kufika Mchuchuma sekondari kupitia njia ya maji/ziwa nyasa yaani Itungi/ Matema -Manda nauli Tsh.10000/-15000/= kisha Manda- Mchuchuma Tsh. 5000/= Meli inapita siku ya Alhamis tu. Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe 06/07/2026. Pia kuripoti shuleni ni 01/07/2026 hadi 14/07/2026

Tahasusi (combination) zilizopo Mchuchuma Sekondari ni CBG,HGK, HGL,

Karibu sana Mchuchuma Sekondari.

THE HEADMASTER
MCHUCHUMA SECONDARY SCHOOL
BOX 43 — LUDEWA

**MICHAEL MATHEW MWALONGO MKUU WA SHULE.**

## 2.0 MICHANGO YA SHULE

**(a)**Mwanafunzi atalipa michango yote kwenye akaunti namba **60101200044, NMB.** Jina la akaunti ni **MCHUCHUMA SECONDARY SCHOOL RECURRENT ACCOUNT.** Tafadhali andika jina la mwanafunzi na mchepuo wake kwenye pay in slip. Pindi afikapo shuleni aiwasilishe kwa mhasibu wa shule.

**(b)**Mchanganuo wa Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi / mlezi wa mwanafunzi ni;-

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1 | Michango ya uendeshaji wa shule | 65,000/= |
| 2 | Tahadhari | 5000/= |
| 3 | Nembo | 5000/= |
| 4 | Kitambulisho cha shule | 5000/= |
| | Jumla | 80,000/= |

**NB:** Michango iliyotajwa hapo juu iwekwe kwenye akaunti ya shule iliyotajwa hapo juu. Kamilisha michango ili kuepuka usumbufu usiokuwa wa lazima.

**(c)** Mahitaji na vifaa muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni:

a) Ream 1 ya karatasi A4 kwa kila muhula (kwa mwaka ream 2). b) Spring file 2

c) Vitabu vya masomo ya tahasusi husika

d) Scientific calculator kwa HGL, HGK na CBG

e) Godoro la futi 2 ½ Dodoma lenye cover yenye ufito pembeni cover lisilo la kuvua,

f) Mashuka jozi 2 rangi ya pinki, na mto kwa wasichana

g) Mashuka jozi 2 rangi ya Blue Bahari na mto kwa wavulana.

h) Net ya kulalia yenye pembe nne

i) Vyombo vya chakula (container la pembe 4 lekundu lenye mfuniko na kijiko)

j) Vindoo viwili kwa matumizi ya mwanafunzi na ofisi.

k) Jembe lenye mpini kwa wanafunzi wa CBG, HGL na HGK.

l) Kwanja moja la kufyekea lililonolewa vizuri.

m) Mwanafunzi wa Combination ya HGK aje na panga moja La kuchonga siyo la dukani lenye mshikio wa mpira, Combination ya HGL Aje na shoka lenye mpini na CBG Waje na spedi yenye mpini wa chuma

n) Mwanafunzi wa kike aje na mkasi wa kukatia maua.

o) Fagio 1 la chelewa kwa kila mwanafunzi.

p) Mopa 1 kwa wanafunzi wa CBG, HGL na HGK.

q) Hard broom 1 kwa wanafunzi wa CBG, HGL na HGK.

r) Soft broom 1 kwa wanafunzi wa CBG, HGL na HGK

s) Toilette brush 1 kwa wanafunzi wa CBG, HGL na HGK

t) Madaftari makubwa kumi 10 aina ya COUNTER BOOK na kalamu za kutosha.

u) Dissection kit 1 kwa watakao soma CBG.

v) Mathematical set moja kwa wanafunzi wa CBG, HGL na HGK.
w) Taa ya solar 1 Kwa dharula ya umeme unapokatika
x) Kila mwanafunzi aje na lita tano ya sabuni ya maji kwa ajili ya usafi wa bwenini Na vyooni

NB: Vifaa kama Magodoro, Ndoo na vifaa vingine vya usafi vinapatikana maeneo yaliyopo karibu na shule.

## SARE YA SHULE.

### WASICHANA

1. Sketi mbili nyeusi esteem no.1 za heshima (linda box) zifike cm 20 chini ya magoti
2. Mashati mawili meupe ya mikono mirefu (tomato)
3. Viatu vyeusi pair 2 visivyo na kisigino kirefu vyenye kamba za kufunga na soksi nyeupe pair 5 au zaidi
4. Sweta rangi ya kijivu mshono wa V shingoni
5. Kwa wanaovaa hijabu, rangi ya hijabu ifanane na sare ya shule yaani nyeupe kwa darasani na dark blue kwa sare za nje (shamba dress).
6. Nguo za kushindia ( Shamba dress ) sketi mbili dark blue ( Esteem No. 1) ndefu za Heshima zifike usawa wa soksi ziwe na malinda ya kawaida kumi (10) na Tshirt 2 za kola za kijivu zisizo na maandishi wala nembo yoyote

### WAVULANA

1. Suluari mbili Nyeusi (Esteem no.1) vipimo upana wa chini cm 15-17 urefu ifike kwenye viatu soksi zisionekane.
2. Shati mbili nyeupe tomato mikono mirefu
3. Viatu vyeusi pair 2 visivyo na kisigino kirefu vyenye kamba za kufunga na soksi nyeusi pair 5
4. Sweta rangi ya kijivu mshono wa V shingoni
5. Nguo za kushindia ( Shamba dress) suluari 2 dark blue esteem no.1 vipimo sawa na sare za darasani na Tshirt 2 zenye kola rangi ya kijivu isiyo na maandishi wala nembo yoyote
6. Mkanda wa kuvalia suluari mweusi wa ngozi
7. Mwanafunzi wa kiume uje na daruga au njumu kwaajili ya michezo.

### SARE YA SHULE:



**CLASS UNIFORM**



**SHAMBA DRESS**



**TRACK SUIT**

**MAHITAJI KWA WOTE**

1. Nguo za michezo (Track Suit ya rangi ya Kijuvu yenye mistari myeupe isiyo na kofia kwa wote pamoja na raba za michezo)
2. Jezi za michezo za rangi ya blue bahari kwa combination ya CBG, Jezi za michezo za rangi nyekundu kwa combination ya HGK na Jezi za michezo za rangi nyeusi kwa combination ya HGL.
3. Sanduku imara la kutunzia vitu vyake (Tranka)
4. Nakala ya matokeo ya kidato cha nne ( Result slip) na nakala ya cheti cha kuzaliwa
5. Aje na Lab. coat 1 kwa wanafunzi wa CBG
6. Aje na Bima kwaajiri ya matibabu inapobidi.

**ZINGATIA**

Mwanafunzi haruhusiwi kuvaa nguo za nyumbani katika maeneo la shule na awapo safarini wakati wa kwenda na kurudi toka likizo avae track suit iliyoagizwa hapo juu. o Suruali za mitumba na jeans haziruhusiwi kabisa shuleni.

- Kila mwanafunzi awe mlinzi wa mali zote za shule na binafsi o Uharibifu wowote utakaotokea ni jukumu la mwanafunzi na mzazi kulipa.
- Kila mwanafunzi azingatie na kufuata maelekezo ya wataalamu wa afya ili kujilinda dhidi ya magonjwa mbalimbali kama IMPOX.

**MAWASILIANO TOKA KWA MZAZI/MLEZI**

**i.** Taarifa zote zinazomhusu mwanafunzi mfano taarifa ya kufiwa itumwe kwa Mkuu wa shule au walezi wa wanafunzi ambao wanatumia simu za shule. **ii.** Utumaji wa fedha kwa wanafunzi kutumia mitandao ya simu zitumwe kwenye simu za shule tu na sio kwa mwalimu yeyote au mtu mwingine yeyote.

**Namba hizo ni:**

1. 0756524162/0776524162 **MICHAEL MWALONGO.** MKUU WA SHULE
2. 0676815962/0615408462 **GEORGE ISAACK LUBUNGA.** MWALIMU WA MALEZI
3. 0657179419 **ERICK MSOLA**. MAKAMU MKUU WA SHULE
4. 0717 719 949/ 0758 282 068 HAWA MWASENGA MAKAMU MKUU WA SHULE

**SHERIA ZA SHULE**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na,

**3.1 Sheria na Kanuni za Shule**

- **i.** Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
- **ii.** Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
- **iii.** Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
- **iv.** Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
- **v.** Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
- **vi.** Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
- **vii.** Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
- **viii.** Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
- **ix.** Kutunza mali za shule;
- **x.** Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
- **xi.** Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- ✞ Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;

- ✞ Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;

- ✞ Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalumu toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).

**MAKOSA YANAYOWEZA KUSABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

**1.** Wizi

**2.** Uasherati, ubakaji na ushoga

**3.** Ulevi wa pombe na madawa ya kulevya

**4.** Uvutaji wa bangi, sigara

**5.** Kupigana, kupiga au kumpiga mwalimu au mtumishi

**6.** Kuoa/kuolewa

**7.** Kusababisha au kupata mimba ndani na nje ya shule

**8.** Kutoa mimba/kusaidia kutoa mimba

**9.** Kutoa lugha chafu/ matusi

**10.** Kudharau bendera ya taifa

**11.** Kuharibu kwa makusudi mali ya umma

**12.** Kupatikana na makosa ya jinai

**13.** Kugoma au kuchochea au kuongoza mgomo shuleni

**14.** Kukataa adhabu halali kwa makusudi

**15.** Kutohudhuria vipindi kwa muda wa miezi miwili bila sababu

**16.** Kupatikana na simu na vifaa vyake, pamoja na kamera au vifaa vyote vitumiavyo umeme

**17.** Kutoroka shuleni mchana au usiku

**18.** Kuchezea miundombinu mathalani umeme, maji, vyoo n.k

**19.** Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni

## Viambatisho na Fomu Muhimu

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;

ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;

iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na

iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

***Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.***

**SHULE YA SEKONDARI MCHUCHUMA**

**FOMU YA MAPATANO /KUKUBALI NAFASI YA MASOMO KIDATO CHA TANO MWAKA 2025**

**A. MWANAFUNZI**

JINA LA MWANAFUNZI ………………………………………………………… ANUANI

…………………………………………………….

Mimi…………………………………………………. Nimekubali/sikubali kujiunga na jumuiya ya shule ya sekondari Mchuchuma. Nimesoma maagizo ya shule kwa makini na kuyaelewa. Naahidi kuwa mtiifu na nitazingatia sheria, kanuni na taratibu za shule, endapo nitakiuka taratibu nichukuliwe hatua za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kufukuzwa shule kadili sheria zinavyo ainisha.

Saini ya mwanafunzi ……………………………..

Tarehe …………………

**B. MZAZI/MLEZI**

Mimi……………………………………………………………………………… Mzazi/Mlezi wa

……………………………………………………….. Nimesoma kwa makini maagizo ya shule yaliyotolewa kwa mtoto wangu.

Nimekubali/Sikubali mwanangu achukue nafasi hiyo. Naahidi kuwa nitashirikiana na uongozi wa shule katika kumkuza na kumlea mwanafunzi huyu kielimu na kitabia. Naahidi pia kumlipia michango mbalimbali iliyoagizwa na shule kwa wakati muafaka. Kinyume chake nichukuliwe hatua za kisheria.

Sahihi ya mzazi ……………………….......................

Tarehe ………………………………..

**OFISI YA WAZIRI MKUU-TAMISEMI**

**TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI**

**Bandika picha hapa**

1. Jina kamili ……………………………………………………………………………

2. Tarehe ya kuzaliwa …………………………………………………..(tarehe, mwezi,mwaka) 3. Kabila …………………………………………. Taifa …………………………………………….

4. Dini na dhehebu ……………………………………………………….. ………………………..

5. Jina la baba ……………………… Hai /Marehemu ………………………..Taifa ………………..

6. Anuani ya baba ……………………………………………… Simu ………………………………

7. Kazi ya baba………………………………………………………………………………………….

8. Jina la mama …………………………………Hai/Marehemu ………………………………………..

9. Wazazi wanaoishipamoja au wametengana …………………………………………………………

10. Jina na anuani ya mlezi wako (Kama si mzazi) ……………………Simu………..………………

11. Wakati wa likizo utakuwa kwa nani na wapi(Taja sehemu moja utakayo kwenda kila wakati na Anuani) ……………………………………………………………………………………………

12. Ndugu au jamaa wa karibu ambao wataruhusiwa kumtembelea au kuwakilisha mzazi/mlezi inapotokea dharula.

| **S/N.** | **JINA** | **ANAKOISHI** | **NAMBA YA SIMU** |
|---|---|---|---|
| 1 | | | |
| 2 | | | |
| 3 | | | |

12. Nathibitisha kwamba habari zote nilizotoa hapa ni kweli na sahihi.

Saini ya mwanafunzi …………………………….. ……………………Tarehe ……………………

Saini ya Mzazi/Mlezi ………………………………………………….... Tarehe ……………………

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

**MCHUCHUMA SECONDARY SCHOOL,**
**P.O.BOX 43,**
**LUDEWA**
**DATE: ….…………**

**TO MEDICAL OFFICER**

…………………………………………

**PART A**

**MR/MRS/MISS** …………………………………………….. please examine the above named Student for her/his physical and mental fitness for a full time learning in this school.

The examination should include the following categories:

1. Haemoglobin ………………………………………………………………………………… 2. P.V.Bleeding ……………………………………………………………………………… 3. Eye sight ……………………………………………………………………………… …..
4. Blood pressure ………………………………………………………………………………..
5. Urine for sugar ………………………………………………………………………………….
6. Stool for examination ……………………………………………………………………….
7. Asthma ……………………………………………………………………………………….. …
8. Skin Disease …………………………………………………………………………………….
9. Leprosy …………………………………………………………………………………………….
10. Epilepsy ……..……………………………………………………………………………….
11. Any deformity ……………………………………………………………………………
12. Pulmonary tuberculosis ………….……………………………………………………………….
13. Neurosis …………..………………………………………………………………………
14. Venereal disease ……………………………………………………………………………
15. Other serious diseases ……………………………………………………………………… 16. Pregnancy ……………………………………………………………………………………….

.

PART B

MEDICAL CERTIFICATE (To be completed by Government Medical Officer)

I have examined the above-named student and find that He/She is physically fit/ unfit and mentally fit /unfit for full time schooling.

OTHER COMMENTS

…………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………… Name and Signature ………………………………………….……Designation …………………………Official stamp …………………………… Date…………………………

Thank you



**MWALONGO M THE HEADMASTER**

## ORODHA YA BAADHI YA VITABU KWA KILA SOMO

### A: HISTORY

1. History for advanced secondary schools forms five, Tanzania institute of education (T. I. E) EDITION, 2023
2. History for advanced secondary schools, Tanzania institute of education (T.I.E) EDITION,2025
3. Modern World History by Ben Walsh
4. African in the World History by Nyirenda
5. The Russian Revolution and the Bolshevik Victory by D.C. Heath and Company
6. Major events in the African history by Fr. Kamara.
7. Zamani East African History by B. Ogoti and J.A. Kieban
8. Essentials in Advanced Level Paper 1&2 by Salehe Yassin.

### B: CHEMISTRY

1. Advanced Chemistry Review by William W. Davis (Mzumbe book shop project, 2004)
2. Physical chemistry by Delungu, et (Mzumbe book shop project, 1998)
3. Advanced Level Inorganic Chemistry part I and II.(Tanzania in state of education,1995)
4. Organic Chemistry volume I. The Fundamental Principles by I.L. Finar (Long man Ltd 1990)

### C. BASIC APPLIED MATHEMATICS

1. Basic applied mathematics for form V and VI by Tanzania institute of education (T.I.E)
2. Scientific calculator f(x) = 991

**D. HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI 1. Kitabu cha historia ya Tanzania na maadili kidato cha tano, Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) Toleo la 2023**

**2. Kitabu cha Historia ya Tanzania na Maadili kidato cha sita, Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) Toleo la 2023**

### E: ENGLISH.

1. English for advanced secondary schools. Students book form five by Tanzania institute of education (T. I. E)
2. English for advanced secondary schools. Students bookform sixby Tanzania instituteof education (T. I. E)
3. Advanced level English Language one Form five and Six by Shadrack and James Kinunda.

4. English. For Advanced level by Dr. M. Kadeghe
5. Advanced English Dictionary – Oxford University

**NOVEL**

1. **Animal Farm by George Orwell -2024**
2. **Chasing the Leopard Finding the Lion by Julie Wakeman Linn – 2024**
3. **The Opportunist Elite by Nyamabri C.M Nyangwine – 2023**
4. **The Horizon Unveiled by Fellowes Mwaisela – 2011**

**PLAY**

1. **The Government Inspector by Nikolai V. Gogol – 2024**
2. **An Enemy of the people by Henrik Ibsen – 2024**
3. **A taste of Heaven by Farouk Topan – 2023**

**POETRY**

1. **Summons poem From Tanzania by Richard S. Mabala - 2023**
2. **Poets of Africa Lament of the Silent & Other poems by Jared Angira - 2024**

**F: KISWAHILI**

1. Sarufi ya Kiswahili Sekondari na Vyuo (Mdee) DUP-DSM
2. Kamusi ya Kiswahili Sanifu–TUKI.
3. Nadharia ya lugha kidato chatano na sita na elimu ya juu (2016) na M.C. Saluhaya

RIWAYA

1. Dunia uwanja wa Fujo – Euphrase Kezilahabi – 2007, Toleo jipya la 2023
2. Ua la Faraja – W.E Mkufya 2007
3. Mirathi ya Hatari – C.G. Mung'ong'o – 2023
4. Wasifu wa siti Binti Saad Shaaban Robert - 2023

TAMTHILIYA

1. Mukwava wa Uhehe – M.M. Mlokozi - 2023
2. Shujaa Milambo – Emmanuel Mbogo - 2023
3. Usaliti Mjini – Francis Imbuga – 2024

USHAIRI

1. Fumbo linanoelea – Nyambari C.M. Nyangwine - 2023
2. Malenga wa ziwe kuu – Wallah Bin Wallah - 2024
3. Andamo, Msafiri Safari – Mohammed Khelef Ghassani – 2023
4. Wosia wa Baba – Ahmed Mohamed Amanzy - 2024

**G: GEOGRAPHY**

1. Practical geography for east Africa by D. M Sagata
2. Research methodology by C.R. Kothari
3. Practical geography for Africa by J.M. Pritchard
4. Human and economic geography by G. Morgan
5. Human geography by Tanzania institute of education (T.I.E)
6. Practical geography for advanced secondary schools Tanzania in statute of education (T.I. E)
7. Physical geography for advanced secondary schools Tanzania in stitute of education (T.I. E)
8. Physical geography in diagrams 4th edition by R.B. Bunnett
9. Practical geography in diagrams by R.B. Bunnett

**H: BIOLOGY**

1. Rwehumbiza, R (2016). Complete advanced biology form five. TVTA Dar Es Salaam
2. Rwehumbiza, R (2016). Complete advanced biology form six. TVTA Dar Es Salaam
3. T.I.E (2019) Biology for Advanced level Secondary schools. Form Five. T.I.E Dar Es Salaam
4. T.I.E (2019) Biology for Advanced level Secondary schools. Form Six. T.I.E Dar Es Salaam
5. Taylor D.J, Green, N.P.O, Stout, G.W (1997) Biological science (3rd ed) Cambridge university press: U K
6. Toole, S.Toole, G (2014) Biology for advanced level (4th ED) Oxford University Press: Uk
7. Dissecting Kit.

**KAULI MBIU YA SHULE “SCHOOL MOTTO” ELIMU NI UKOMBOZI.**

Kauli hiyo ndiyo itakuwa dira ya mwanafunzi wakati wote atakapokuwa hapa shuleni kwa kipindi chote cha miaka miwili. Mwanafunzi anatakiwa kuitafakari kauli mbiu hiyo kwa vitendo. Nimatumaini yetu kuwa

Mwanafunzi atatumia nafasi hii adimu kwa manufaa yake na kwa Taifa kwa ujumla. Hivyo basi, atatakiwa kuwa na tabia njema na uhudhurie masomo na kujifunza kwa bidii

**TUNAKUTAKIA SAFARI NJEMA**